

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

(Barua zote ziadikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu Na. 023 2440164
Nakishi. 023 2440338

E - MAIL:
dedchalinze@pwani.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 65,
CHALINZE.

29/08/2017

Ukijibu tafadhali nukuu:
Kumb. Na. HWC/S.20/VOL.I/769

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze kupitia kibali cha ajira Chenye Kumb. Na. FA170/375/01/46 cha tarehe 31 Julai, 2017 na kibali chenye Kumb. Na. CFC 26/205/01 "FF"/91 cha tarehe 22 Agosti, 2017 anawatangazia Wananchi wote wenye sifa za Muundo wa kazi zifuatazo:-

**1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III NAFASI 41 – NGAZI
YA MSHAHARA NI TGS B**

MWOMBAJI AWE NA SIFA ZIFUATAZO:-

Mwombaji awe na elimu ya Kidato cha Nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/ Cheti katika fani zifuatazo:

- Utawala,
- Sheria,
- Elimu ya Jamii,
- Usimamizi wa fedha,
- Maendeleo ya Jamii,
- Na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI/MAJUKUMU

- i. Atakuwa Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Atakuwa msimamizi Mkuu wa Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, atakuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Ataratibu na Kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Atakuwa Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika kijiji.
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji.
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
- xiii. Kazi nyingine zote atakazopangiwa na Mwajiri.

MASHARTI YA AJIRA

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye umri wake usiopungue miaka 18 na kuzidi miaka 45.
- ii. Mwombaji lazima aambatanishe wasifu binafsi (CV) wenye mawasiliano ya uhakika anuani, barua pepe na namba za simu,
- iii. Mwombaji aombe kwa kufuata tangazo hili la kazi,
- iv. Mwombaji lazima aambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
 - a) Astashahada/cheti cha utaalum kulingana na sifa za nafasi husika,
 - b) Cheti cha Mtihani wa kidato cha nne au sita,
 - c) Cheti cha kuzaliwa.

- v. Hati ya matokeo ya kidato cha nne (Result slip) haitafanya kazi,
- vi. "Transcript" ambayo haikuambatanishwa na cheti haitafanya kazi,
- vii. Kuwasilisha vyeti vya kughushi na maelezo mengine itasababisha kuchukuliwa hatua za kisheria.
- viii. Mwombaji ambae ni Mtumishi wa Umma haruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- ix. Mwombaji aliyestaafu kazi kwa sababu yoyote ile haruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- x. Hajawahi kufukuzwa kazi Serikalini.
- xi. Hajawahi kufungwa kwa makosa ya jinai.
- xii. Mwombaji aonyeshe wadhamini wawili na mawasiliano yao anuani na namba za simu.
- xiii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.
- xiv. Aambatanishe picha 2 za Passport Size za hivi karibuni.


Maombi yatumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE,
S.L.P 65.
CHALINZE.

Mwisho wa kutuma maombi ni **tarehe 14 Septemba, 2017 saa tisa na nusu (9:30) Alasiri.**

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-

.....
EDES P. LUKOA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE



Nakala:

Mbao za Matangazo